

FASIHI YA KISWAHILI NA MUZIKI WA ZILIZOPENDWA: UKOMBOZI WA KISIASA
AFRIKA

Elizabeth Mahenge
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Makala hii inachambua dhamira ya mapambano ya kujikomboa kati ya Waafrika na wakoloni waliowatawala kisiasa katika bara la Afrika. Nyimbo za zamani, hasa muziki wa zilizopendwa zitachunguzwa ili kubainisha jinsi dhamira ya ukombozi wa kisiasa inajitokeza. Hii ni pamoja na kuzingatia jinsi zinabainisha harakati za mapambano ya kujikomboa, mbinu za mapambano na mafunzo tunayopata kutokana na sanaa hii.